Jumatatu
15 Februari 2021
www.timesmajira.co.tz

Ruvuma wajipanga kudhibiti kilimo kwenye vyanzo vya maji ili kulinda mazingira, afya

Na Albano Midelo

KIKAO cha wadau wa maji mkoani Ruvuma kikiongozwa na mkuu wa mkoa huo kimeptisha azimio la kufanya operesheni kabambe ya kuwaondoa wote waliovamia vyanzo vya maji, vitendo vinavyosababisha athari kwa mazingira.

Mwenyekiti wa kikao hicho, Mkuu wa Mkoa (RC) Ruvuma, Chnstina Mndeme, alisisitiza kuwa, ambao walishalima kwenye vyanzo vya maji ambamo mimea imeshaota, huu itakuwa ni msimu wa mwisho kulima maneno hayo.

"Tutaendesha operesheni ya kuwaondoa wale wote ambao wanakwenda kulima kwenye vyanzo vya maji na kusababisha watu wengine wapate maji machafu, hii halikubaliki, lazima waondoke," RC Christina alisema katika kikao hicho.

Aliagiza wenyeviti wa halmashauri zote nane mkoani humo kwamba, wahakikishe kuwa suala la kuwaondoa waliovamia vyanzo vya maji inakuwa azimio katika vikao vya baraza la madiwani.

RC Christina alisema kuwa, ambao wameshalima mahindi kwenye vyanzo vya maji hivyo, ambamo tayari mimea yake imeshaanza kukua na walishaweka mbolea, msimu huu senkali hataamuru ing'olewe.

Alitahadharisha kwamba, kilimo kwenye vyanzo vya maji kwa kutumia mbolea zenye kemikali husababesha madhara makubwa kwa watumiaji wa maji hayo, ambao huyanywa wakati huwa tayari yana kemikali za mbolea, hivyo huweza kusababesha athari za kafya kwao.

Kutokana na matuko hayo, RC Christina aiomba wadau wote wa maji wasambaze uelewa kwa wanajamii kuhusu athari za kuvama vyanzo vya maji, aksisitiza kwamba, kuanza mwakani mtu yeyote ambaye atafanya shughuli za kiuchumi kwenye vyanzo vya maji atafikishwa kwenye mamlaka zinazosimamia Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 pamoja na Sheria za Maji za Mwaka 2002 na Mwaka 2019.

Pia, RC Christina aliagiza maafisatarafa pamoja na viongozi wote ngazi za wilaya kwamba wasimamie utunzaji wa vyanzo vya maji ili visiathirwe.

Maagizo mengine aliyotoa mkuu wa mkoa hayo katika kikao hicho ni kwamba, halmashauri zote na sekretarieti ya mkoa wawajibike kikamilifu kutekeleza na kusimamia majukumu yote yaliyoorodheshwa kwenye Sheria Namba Tano (5) ya Huduma ya Maji ya Mwaka 2019.

"Mameneja wa RUWASA wilaya, kwa kushirikiana na halmashauri zote, zihakikishe kwamba, miradi iliyopo na mingine itakayojengwa, inaunda vyombo huru vya watumiaji maji kwa Sheria Namba Tano ya Mwaka 2019 kabla au ifikapo Mei 31, 2021," aliagiza.

RUWASA ni Wakala ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini Mkoa wa Ruvuma.

Vilevile, RC Christina aliagiza kwamba, katika kikao cha baraza la madiwani ambacho hutanyika kila robo mwaka kuwa, kwenye halmashauri zote kwepo mada ya kudumu ambayo mameneja wa RUWASA katika wilaya husika watatoa taarifa kuhusu hali ya upatikanaji na usafi wa vyombo vya watumiaji maji.

Pia, aliagiza RUWASA wilaya na mkoa kwamba washirikiane na Mamlaka ya Maji na Majitaka Songea Mjini (SOUWASA) pamoja na ofisi za mabonde ya maji ili kutafuta vyanzo vya maji na kuandaa mpango ya utunzaji wa vyanzo vya maji.

Akiendelea kuagiza: "Naagiza fedha zitokanazo na mauzo ya maji zikaguliwe na mkaguzi wa ndani wa halmashauri, ili kujindhisha namna fedha hizo zilivyotumika.

"Endeleeni kuwachukulia hatua wanaoharibu kwa makusudi miundombinu ya maji na vyanzo vya maji."

Odo Mwisho, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Ruvuma, akizungumza kuhusu uharibifu wa vyanzo vya maji unavyoendelea mkoani Ruvuma, amesema kuwa kuharibu vyanzo vya maji itasababesha madhara makubwa ya kimazingira kwa watu wote.

Mwisho anasema viongozi wa serikali wanapotekeleza wajibu wao wa kusimamia utunzwaji wa vyanzo vya maji, viongozi wa kisiasa imekuwa hutetea wananchi wanaoathiri mazingira, kwa kutamka "ni wapigakura wetu."

"Nilogu wanasiasa wenzangu, tuache mzaha katika suala la mazingira, tutavuna mabua, tutawaangamiza wananchi kwa sababu mwisho wa siku, kama sio kizazi hiki, basi kizazi kijacho kitapata matatizo makubwa sana ya kimazingira."

Mwisho amesisitiza kwamba suala la kusimamia utunzwaji wa vyanzo vya maji lipewe kipaumbele, kuwa wote waliovama na kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi waondolewe.

"Nilogu wanasiasa wenzangu tusijipendekeze kwa wananchi katika suala hili, jambo ambalo litakuja kuleta athari kubwa kwa wananchi.

"Tuchukue hatua, na sisi tuendeloe kuwaelimisha wananchi umuhimu wa vyanzo vya maji kwa maisha endelevu," amesema Mwisho.

Meneja wa RUWASA Ruvuma, Mhandisi Rebman Ganshonga ametaja jambo moja ambalo dira na sayansi havipingani, kwamba ni nadhana ya maji kuwa chanzo kikuu cha uhai wa viumbehai wote, ikiwemo binadamu, wanyama na mimea.



Mkuu wa Mkoa Ruvuma, Christina Mndeme, alipokuwa akiongoza kikao cha wadau wa maji mkoani humo. (Picha Mpigapicha Wetu)

Mkuu wa Mkoa Ruvuma amesema kuanzia mwakani hakuna mtu yeyote ambaye atafanya shughuli za kiuchumi kwenye vyanzo vya maji ...

Kutokana ni jukumu hilo Mhandisi Ganshonga anashauri wadau wote wa maji, ikwemo wananchi wenyewe, kwamba watunze vyanzo vya maji na mundombinu yake kwa manufaa yao wenyewe kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Akizungumzia majukumu yaRUWASA, Mhandisi Ganshonga ametaja kuwa ni kusimamia huduma za maji vijijini, kuandaa mipango ya kusanifu miradi, kujenga na kusimamia utekelezwaji wake.

Kwamba jajukumu mengine ni kuendeleza vyanzo vya maji kwa kufanya tafiti za maji chini ya ardhi, kuchimba visima na kujenga malbwawa, na kufanya matengenezo makubwa ya miundombinu ya maji.

Mhandisi Ganshonga ametaja majukumu mengine kuwa ni kuenoza uelewa kuhusu usafi wa mazingira katika ngazi za kaya na mtubwitafu, pamoja na masuala ya uhifadhi na utunzwaji vyanzo vya maji, kuwawezesha kuwezo wanajamii kuhusu uender .aji na matengenezo ya mra a maji vijijini.

RUWASA ilianzishwa kwa Sheria Namba Tano ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019.

Scanned with CamScanner